TANGAZO LA SERIKALI Na. 1076 la tarehe 20/12/2024

SHERIA YA USIMAMIZI WA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE GARI MOJA LA MRADI WA TAIFA WA KUDHIBITI MALARIA KWA WIZARA YA AFYA YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye Gari Moja la Mradi wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kwa Wizara ya Afya ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika tarehe 13 Novemba mwaka 2024.

Msamaha

**2**. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi cha shillingi 152,543,400 cha ushuru wa bidhaa kinachopaswa kulipwa kwa gari moja lililoainishwa katika Jedwali linaloingizwa ndani ya nchi au kununuliwa, kabla ya kibali kupitia forodha na au kwa niaba ya Wizara ya Afya kwa ajili ya kutumika katika Mradi wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kimesamehewa.

Masharti

**3**. Msamaha wa ushuru unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa, iwapo gari husika litatumika kwa matumizi tofauti, litahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kupata manufaa yanayotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

**4**. Amri hii itafikia ukomo tarehe 13 ya mwezi Mei, mwaka 2025.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Injini | Namba ya Chassis | Idadi | Eneo la Ununuzi Ndani ya Nchi/Nje ya Nchi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Land Cruiser Hardtop, 5 doors | 1HZ-1077551 | JTEEB71 J10F031220 | 01 | Nje ya Nchi |

Dodoma,
13 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*